



Mfwa Bwacha
Tebuka
12/2/16

**MABADILIKO YA BODI YA VILEO KUWA
MAMLAKA YA LESENI:**

1.0. UTANGULIZI:

Kwa mujibu wa sheria ya liseni za vileo na 28 ya 1968 iliyounda bodi ya vileo na sheria Na 12 ya 1978 na marekebisho yake ya 1982 na 2002 kifungu Na 3 (a) ilivunja Bodi za vileo na kuunda Mamlaka ya leseni za vileo na mwongozo wa utekelezaji kutolewa na serikali mwaka 2011.

1.1. MUUNDO WA MAMLAKA YA LESENI:

Muundo wa Mamlaka ya leseni za vileo utakuwa kama ifuatavyo:-

- | | |
|-------------------------------|--------------|
| 1. Mhe. M/kiti wa Halmashauri | - Mwenyekiti |
| 2. Afisa Biashara | - Katibu |
| 3. Wah. Madiwani watatu | - Wajumbe |
| 4. Afisa Afya | - Mjumbe |
| 5. Afisa Utamaduni | - Mjumbe |
| 6. Afisa mipango miji | - Mjumbe |

Wajumbe wanaoweza kualikwa

1. Kamanda wa polisi Wilaya.

2.0. MAJUKUMU YA MAMLAKA YA LESENI ZA VILEO:

2.1. Vikao vya Mamlaka:

Mamlaka yenyewe itapanga siku yeyote ndani ya mwezi Septemba (kipindi cha kwanza na ndani ya mwezi Machi (kipindi cha pili) ili kujadili maombi ya Leseni za vileo kwa ajili ya kipindi cha miezi sita itakayoanzia Oktoba au Aprili au inaweza kupanga tarehe nyingine yoyote itakayoona inafaa 38 (1).

2.2. Kupokea maombi:

Maombi yote ya biashara za vileo yatapokelewa na Mamlaka kwa muda utakaopangwa 36 (1).

itendegui'sclory@gmail.com

2.3. **Maoni ya wadau:**

Orodha ya majina ya waombaji na sehemu wanazofanyia biashara yatabandikwa kwenye ofisi ya Mamlaka ya leseni ya vileo na maeneo mengine husika, wadau (wakazi) au raia yeyote wataruhusiwa kutoa maoni kukubali au kukataa kuhusiana na maombi hayo.

2.4. **Kujadili maombi:**

Maombi yatajadiliwa na Mamlaka teule ya leseni za vileo. Mjumbe yeyote mwenye maslahi katika uuzaji wa vileo hataruhusiwa kuhudhuria kikao cha kupitisha maombi mapya na/au marudio ya maombi 4 (2).

2.5. **Matokeo ya maombi:**

Mamlaka inaouwezo kamili wa kukubali au kukataa maombi ya leseni za vileo kwa misingi ya sababu zitakazotolewa na kujadiliwa. Matokeo ya maombi yatatangazwa na Mamlaka kwa kipindi husika.

3.0. **UTARATIBU WA MAOMBI:**

3.1. **Namna ya kuomba:**

Mwombaji atatakiwa kujaza nakala tatu za fomu za maombi zilizoandaliwa na ofisi ya Mamlaka, Kwa ajili ya ukaguzi na utoaji wa maoni ya wataalamu (Afya, Polisi na Mamlaka ya leseni)

1. Kamanda wa Polisi wa Wilaya atapelekewa nakala moja ambayo ataitumia katika ukaguzi na kutoa taarifa kwa maandishi kukubali au kutokubali kupewa leseni na sababu zake. Mamlaka inaweza kumualika Afisa huyo wakati wa kikao cha kujadili maombi hayo.
2. Afisa Afya atafanya ukaguzi kwenye eneo la biashara la mwombaji na atatoa ushauri kwa wajumbe wa kikao cha Mamlaka.
3. Orodha ya majina ya waombaji itabandikwa kwenye ofisi ya Mamlaka ya leseni za vileo na maeneo mengine siku 14 kabla ya kujadiliwa (kifu. No. 37 (3)).

- Mtu yeyote anaweza kuweka pingamizi la kutolewa leseni fulani 39 (1) kwa maandishi akitaja sababu kabla ya kujadiliwa au wakati wa kujadiliwa na Mamlaka.

4.0. MASHARTI YA LESENI:

Baadhi ya masharti muhimu ya leseni ya biashara za vileo ni kama yafuatayo:-

1. Leseni ya vileo haitatolewa kwa mtu aliye na umri wa chini ya miaka 21.
2. Mtu yeyote ambaye leseni yake imefutwa, hatapewa tena leseni hadi baada ya miaka 2 kupita.
3. Mtu yeyote akibainika anaendesha biashara kwa kutumia leseni iliyokwisha muda wake atafungiwa.
4. Leseni haitatolewa kwa mtu yeyote aliyewahi kufungwa kwa kipindi chochote kinachozidi miezi 6.
5. Ni marufuku kwa mwenye leseni kuruhusu mtoto wa chini ya miaka 16 kuuza pombe, kuajiliwa au kuingia ndani ya eneo linalouza pombe.
6. Sehemu zilizoruhusiwa kunywesha pombe haziruhusiwi kuuzwa kitu kingine chochote eneo hilo bila ruhusa ya maandishi toka kwa Mamlaka ya leseni, isipokuwa vinavyohusiana na hotel au migahawa na viburudisho kama sigara.
7. Hifadhi za vileo (stoo) zote kwa ajili ya kuuza ziwe zimekaguliwa na kuruhusiwa na Mamlaka ya leseni.
8. Ulevi uliozidi na tabia zisizo za kistaarabu au kushawishi, kuendelea kumpa mtu aliyelewa kilevi zaidi katika eneo la biashara hairuhusiwi.
9. Kila mfanyabiashara wa vileo lazima awe na leseni ya vileo iliyotolewa na Mamlaka ya vileo kwa kipindi aliloruhusiwa.

10. Leseni ya vileo ni lazima iwekwe wazi, sehemu inapoweza kuonekana kwenye eneo la biashara aliloruhusiwa.

11. Mwenye leseni atabandika jina lake na aina ya unyeshwaji na biashara katika eneo la biashara aliloruhusiwa.

5.0. AINA YA LESENI, ADA NA MUDA WA KUUZA VILEO:

Lifuatalo ni jedwali linaloonyesha aina ya leseni, uuzaji unaotakiwa, ada ya maombi ya leseni muda (masaa) ya kunyeshea kama ilivyo katika sheria na waraka wa leseni za vileo;

Na.	Aina ya leseni	Aina ya uuzaji unaotakiwa	Ada	Muda wa kuuza	
				Siku za kawaida	Weekend na sikukuu
1.	Wholesale dealers licence	Mtu anunua pombe kwa jumla na kwenda kuuza mahai pengine	22,000/=	2:00 asubuhi - 1:00 jioni	3 asubuhi - 6 usiku
2.	Retailer's off licence	Rejareja, mnunuzi asinywee hapo	32,000/=	2:00 asubuhi - 1:00 jioni	3 asubuhi - 6 usiku
3.	Retailer's on bar licence	Rejareja na mnunuzi kunywa eneo la mwanaji kusika tu	42,000/=	12 jioni hadi 5 usiku	5 asubuhi - 6 mchana 12 jioni - 6 usiku
4.	Hotel licence	Kwa ajili ya wageni tu waliochukua vyumba na kuorodhesha majina yao kwenye kitabu cha wageni	42,000/=	Masaa 24	Masaa 24
5.	Restaurant licence	Kwa mtu anayekula chakula tu	42,000/=	6:00 mchana - 8:00 mchana 12 jioni - 6 usiku	6:00 mchana - 8:00 mchana 12 jioni - 6 usiku
6.	Combined hotel and retailer's on licence	Kwa ajili ya wageni waliochukua vyumba na kuorodhesha majina yao kwenye kitabu na wasiojiorodhesha.	24,000/=		
7.	Club licence	Kuuza pombe na spirit kwa wanachama wa club tu.	24,000/=	12 jioni - 5 usiku	5 asubuhi - 6 mchana 12 jioni - 6 usiku
8.	Club beer licence	Kuuza pombe tu na sio spirit kwa wanachama wa club tu.	20,000/=		
9.	Canteen licence	Kunyweshea eneo lililoruhusiwa	5,000/=		
10.	Temporary intoxicating liquor licence.	Kunyweshea eneo lenye tukio husika	4,000/=	6 mchana - 8 mchana 11 jioni - 6 usiku	5 asubuhi - 6 mchana 12 jioni - 6 usiku


Godfrey Machumu
KATIBU
MAMLAKA YA LESENI ZA VILEO